BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 10 Mei, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 04 Machi, 2023.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2023/2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

106. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kufuatia hali ya uvunjifu wa amani na uwepo wa vitendo vinavyopelekea kumong'onyoka kwa maadili katika shehia mbali mbali mjini na mashamba ndani ya Zanzibar, shehia nyingi zimeanzisha vikundi vya Polisi Jamii ambavyo vina miongozo inayotambulikana na wananchi na Ofisi za Polisi za Wilaya na Mikoa. Hata hivyo, vikundi hivi vimekuwa vikifanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi.

(a) Je, ni msaada gani ambao Serikali inautoa kwa vikundi hivi vya Polisi Jamii kwenye shehia husika.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na utaratibu wa kuwapa wafunzo wananchi wanaojitolea kuunda vikundi vya Polisi Jamii.

(c) Je, vikundi hivi vya Polisi Jamii vinaweza kuingizwa katika mpango wa wanufaika wa mikopo ya Serikali yenye masharti nafuu.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

38. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kwa kuwa Serikali kupitia programu zake za uwezeshaji imefanikiwa kuwapatia mafunzo wananchi 4,171 kwa Unguja na Pemba.

(a) Je, ni watu wangapi wenye ulemavu kwa Unguja na Pemba wameweza kushiriki katika mafunzo hayo.

(b) Je, kati ya hao, wanawake wangapi wameshirikishwa katika mafunzo hayo.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

40. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba vimezungukwa na bahari ya Hindi na walinzi wa mipaka yetu ni Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM). Na kwa kuwa tunashuhudia kuwa Kikosi cha KMKM kinafanya kazi vizuri kwa kukamata magendo na kutoa taarifa za kazi zake hizo kwenye vyombo vya habari.

(a) Je, kwa sababu gani maamuzi ya kesi za watu hawa wanaokamatwa hayasikiki katika vyombo vya habari.

(b) Je, ni sababu gani zinazopelekea watu wanaokamatwa na KMKM ikiwa ni pamoja na wahujumu uchumi huonekana nje siku ya pili tu bila ya kutumikia kifungo.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

16. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Pamoja na kuwepo kwa mifumo mbali mbali ya ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa mapato hayo, bado kumekuwa na upotevu mkubwa wa fedha za Serikali kupitia mifumo hiyo.

Je, ni upi mkakati wa Serikali katika kudhibiti fedha za wananchi zisiendelee kupotea.

<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>

26. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nane imeanza kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo nchini.

Je, kwa nini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hafanyi "*Real Time Auditing*" kwenye miradi hiyo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

54. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Wizara yako katika kuhakikisha usalama barabarani unapatikana, bado kuna tatizo la baadhi ya wananchi kujiwekea matuta kiholela na kusababisha ajali zisizokuwa za lazima.

(a) Je, Wizara yako inafuatilia vipi taarifa za uwekaji wa matuta unaofanywa na wananchi hao katika maeneo mbali mbali ya barabara zetu.

(b) Je, inakubalika vipi wananchi kujiwekea matuta kiholela badala ya matuta hayo kuwekwa na Wizara yako pekee.

(c) Ni hatua zipi zinazochukuliwa na Wizara yako kwa wananchi wanaojiwekea matuta kiholela.

**Wizara ya Afya:**

2. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaohudumiwa, Kituo cha Afya cha Pandani kimekuwa kidogo sana kukidhi haja ya uanzishwaji wake. Aidha, kituo hicho ni kibovu sana, chenye dari iliyoanguka na kuvuja kupita kiasi, huku kukiwa na wafanyakazi watatu tu wanaowahudumia wananchi wasiopungua 7,350.

Pamoja na kwamba wafanyakazi wa kituo hicho wenye stashahada (diploma) wamefanya kazi kwa zaidi ya miaka 30, inasikitisha kwamba marekebisho mapya ya mishahara yamewaweka kwenye ngazi na kiwango cha malipo ya chini ukilinganisha na wafanyakazi wa vituo vyengine wenye astashahada (certificate) tu na wasio na umri mkubwa wa kazi.

(a) Je, ni kwa nini Serikali haikihudumii ipasavyo Kituo cha Afya cha Pandani na wafanyakazi wake.

(b) Je, ni vigezo vipi vimetumiwa na Serikali katika kuwapandisha wafanyakazi wenye astashahada (certificate) tu na wasio na umri mkubwa wa kazi na kuwateremsha wafanyakazi wenye stashahada (diploma) na umri mkubwa wa kazi.

(c) Je, ni upi mpango wa muda mfupi na wa muda mrefu wa

Serikali wa kukifufua na kukitanua Kituo cha Afya cha Pandani.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

31. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Msingi ya Mchangamdogo (Mchangamdogo Primary School) ina wanafunzi zaidi ya 250, lakini inakabiliwa na upungufu mkubwa wa mabanda ya kusomea. Katika skuli hiyo, kuna banda lenye vyumba vinne ambavyo ni chakavu mno na ni hatari kwa usalama wa wanafunzi pamoja na walimu wao na tayari chumba kimoja cha banda hilo kimeshaanguka na wanafunzi wamehamishwa na kusomea katika maeneo yasiyoridhisha. Jambo hili linaleta usumbufu mkubwa sana kwa wanafunzi.

(a) Je, ni lini Wizara yako itatatua changamoto ya madarasa katika skuli hiyo.

(b) Kwa kuwa fedha za COVID zimetumiwa na Serikali katika maeneo kadhaa kujenga miradi mbali mbali ya maendeleo, je, ni lini Serikali itazitumia fedha hizo kutatua changamoto ya madarasa katika skuli ya msingi ya Mchangamdogo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

11. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa Dunia hivi sasa inajikita katika suala la kujifunza lugha ya Kiswahili.

Je, kwa mwaka 2021/2022 ni wageni wangapi ambao wamefanikiwa kujifunza lugha ya Kiswahili na kupatiwa vyeti vya ufaulu kwa lugha hiyo hapa Zanzibar.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

1. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

   Wananchi wa maeneo ya Kombeni na Maungani jimbo la Dimani wamekuwa na changamoto ya kupata umeme mdogo kutokana na nguvu ndogo ya "transformer" iliyopo hospitali ya Kombeni, hali ambayo inaleta shida hasa kwa wajasiriamali wanaotegemea nishati ya umeme katika shughuli zao.

   (a) Je, watendaji wa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) wanafahamu uwepo wa changamoto hiyo.

   (b) Je, ni hatua gani za haraka na dharura ambazo ZECO wamepanga kuzichukua ili kuwasaidia wananchi na wajasiriamali wa Kombeni na Maungani waondokane na athari za umeme mdogo.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2023/2024.

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**

**Zanzibar,**
**10 Mei, 2023.**